

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE

*Barua zote zianjikwe na kutunwa kwa:*

Mkurugenzi Mtendaji (W)

Simu: +255 659 566703 (Direct line)

S.L.P. 70, SIKONGE  
TABORA

*Barua Pepe:* [ded@sikongedc.go.tz](mailto:ded@sikongedc.go.tz)

TAREHE: 08/09/2022

## TANGAZO

### LA

## ZABUNI YA KUTOA HUDUMA YA UKUSANYAJI WA TAKA NGUMU KATIKA SENTA ZA BIASHARA NA MAKAZI KATIKA MGODI WA KITUNDA

### - LGA/121/2022 - 2023/NC/05 - LOT 2

1. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge anakaribisha maombi toka kwa Watu binafsi / Vikundi / Wajasiliamali wenye nia na uwezo wa kutoa huduma ya ukusanyaji wa taka ngumu katika Senta za Biashara na Makazi katika Mgodini wa Kitunda.
2. Waombaji wanakaribishwa kuleta Vidadisi bei kwa ajili ya utekelezaji wa kazi kama ilivyoelezwa kwenye Maelezo ya Mahitaji na Bei kama ilivyofafanuliwa katika Sehemu ya II.
3. Vitabu vya vidadisi bei vinapatikana katika Ofisi ya Manunuzi na Ugavi Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge kwa bei ya Tsh. 15,000/= ambayo haitarudishwa (non - refundable). Mwombaji atalipia kitabu cha Zabuni baada ya kupewa ' Control number / Account number / BILL toka katika Ofisi ya Mwekahazina au Uhasibu na kulipia
4. Vidadisi bei vyote viwe na nakala HALISI (ORIGINAL) na 'COPY' MOJA zinazofanana, zilizojazwa kwa usahihi na zilizowekwa kwenye bahasha zilizowekwa kwenye bahasha na juu yake iandikwe kama ifuatavyo;

**"KIDADISI BEI NA. LGA/121/2022- 2023 /NC/05 LOT 2" KUTOA HUDUMA YA  
UKUSANYAJI WA TAKA KATIKA SENTA ZA BIASHARA NA MAKAZI KATIKA  
MGODI WA KITUNDA**

**LGA/121/2022/2023/NC/05 LOT 2**

5. Maombi yote yapelekwe (yatimwe) **KWA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI  
(W) KITENGO CHA MANUNUZI,**  
**S.L.P 70,**  
**SIKONGE.**
6. Mwombaji atafanya kazi ya kuzoa taka katika sehemu za kukusanyia taka, sehemu za biashara na makazi
7. Mwombaji atafanya kazi ya kusafisha taka na kuzihifadhi sehemu atakayoelekezwa
8. Mwombaji atafanya kazi ya kusafisha Mitaro kandokando ya barabara zote
9. Mwombaji atafanya kazi ya kukusanya tozo za huduma ya kukusanya taka kwa niaba ya Halmashauri kwa kutumia POS
10. Mwombaji / kikundi kitalipa ushuru wa huduma ambao ni asilimia 0.3 na asilimia 5 ya Kodi ya zuio (Withholding tax)
11. Mwombaji aambatishe HATI ya kurandikishiwa kwa Kikundi / Kampuni
12. Mwombaji atakayepata kazi hii atawasilisha mapato yote Halmashauri na kutaja asilimia ambayo atailipa Halmashauri
13. Mwombaji anatakiwa afanye utatiti kwenye eneo la mgodi wa Kitunda kabla ya kuwasilisha maombi ya zabuni anayoiomba
14. Maelezo mengine ambayo mwombaji angepaswa kuzingatia yanapatikana katika kabrasha la zabuni
15. Siku ya mwisho ya kuwasilisha Vidadisi bei ni **siku ya ALHAMISI tarehe 22 .09. 2022 saa 5:00 Asubuhi.** Maombi yatafunguliwa hadharani mara tu baada ya muda wa mwisho wa kupokea maombi. Ufunguzi utafanyika mbele ya wawakilishi wa wazabuni wanaoamua kuhudhuma katika ufunguaji wa zabuni katika ukumbi mdogo uliopo katika jengo la Idara ya Elimu Sekondari
16. Maombi yatakayochelewa, sehemu ya maombi, maombi ya kielektroniki, na maombi yasiyofunguliwa katika tukio la ufunguaji, kwa hali yoyote ile vidadisi bei hivyo havitakubaliwa kwa tathmini.

17. Mwombaji azingatie masharti ya Sheria ndogo za Halmashauri zinazohusiana mapato, ukusanyaji wa taka na usafi wa mazingira. *na sheria mama ya mazingira*

#### JINSI YA KUFANYA KAZI

- i) Wakala atapewa na Halmashauri mashine ya kukusanyia ushuru (POS) na wakati wote wakala atahakikisha anatumia mashine hiyo kukusanya ushuru huo
- ii) Wakala atalipwa asilimia ya makusanyo yake baada ya kuwasilisha makusanyo yake yote kwa mwezi husika
- iii) Gharama ya kulipa wafanyakazi ni juu ya Wakala mwenyewe
- iv) Mwombaji awe na vitendea kazi vya kutosha kufanyia kazi anayoomba
- v) Gharama ya usafishaji na usafirishaji wa taka ni juu ya Wakala mwenyewe



Nico A. Kayange

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
SIKONGE**

**MKURUGENZI MTENDAJI  
WILAYA - SIKONGE**